

Pambazuko

Toleo Namba 063

Jumatatu Februari 26-Machi 3 2024

Mgawo umeme kuwa historia?

•Megawati 235 zaingizwa gridi jana



UK. 12



Mapazia ya 183m/yaning'inia ofisi ya Gachagua

UK. 10

Mtuhumiwa mauaji ya kimbari adakwa

UK. 16

TAHARIRI:
Tusilaani Tanesco, shida ni wanasiasa

UK. 2



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Tusilaani Tanesco, shida ni wanasiasa

WATANZANIA wanalia. Wanasononeka kila uchao kwa madhila mengi; kubwa kwa sasa likiwa ni kukosekana kwa nguvu ya nishati – kwa maana ya umeme.

Wanaolalamikiwa ni Tanesco, shirika la kuzalisha na kusambaza umeme, lakini kadhia hiyo ya kukosekana kwa nishati hiyo muhimu ikitazamwa kwa undani, inabainika kuwa shida siyo shirika hilo, bali serikali.

Inafahamika kuwa Tanesco ina idara maalumu inayoshughulikia mipango na miradi, ndani ya idara hiyo kuna kitengo cha utafiti.

Watendaji waliomo kwenye kitengo hicho kazi yao kubwa ni kubuni vyanzo vipya vya umeme kulingana na mahitaji ya wakati uliopo na ujao.

Tunatambua kuwa idara hii inafanya kazi kubwa na nzuri, lakini tatizo ni kutekelezwa kwa matokeo na mapendekezo yao kwa “wakubwa.”Ni lazima serikali iridhie, kinyume na hapo hakuna kinachofanyika.

Isiyokuwa bahati, kila serikali mpya inapointia madarakani, haina mwendelezo wa mipango iliyopo ya kuongeza vyanzo vya umeme. Inakuja na yake. Ya zamani inaachwa.

Ikumbukwe kwamba wanaohudumu katika idara hiyo ni wataalamu na wamesomea mambo haya, lakini anayeridhia au kukataa ni wanasiasa ambaye siyo mtaalamu wa masuala haya.

Kwamba hivi sasa duniani kote umeme unaozalishwa kwa maji hautegemewi sana kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi, hakuna tena mvua za kutosha kujaza mabwawa makubwa ya maji ya

kuzalisha umeme.

Hapa Tanzania, hizi mvua zinazoonekana kunyesha maeneo ya mijini na hata kusababisha “mafuriko ya kujitakia,” hazina msaada mkubwa katika mabwawa ya umeme.

Kwa kuona hayo, idara hiyo ikapendekeza uzalishaji wa umeme kwa njia ya gesi, na kazi ikaanza kati ya mwaka 2005 hadi mwaka 2010.

Tanesco ilijielekeza kuzalisha umeme kwa njia ya gesi ambapo kupitia mpango huu vituo vifuatavyo vilianzishwa; Kinyerezi I- III, Ubungo I - III na Tegeta Gas Plant. Vituo vyote hivi vinazalisha zaidi ya megawati 1000.

Vyanzo vingi vya maji vya kuzalisha umeme, hasa vilivyoanzishwa na serikali ya awamu ya kwanza, ikiongozwa na Mwalimu Julius Nyerere, baadaye havikuwa na uwezo kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na pia teknolojia, hivyo kuanza kuachana na njia hizo.

Serikali zilizofuata zikiiongozwa na Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete, zikaweka nguvu katika miradi ya gesi, hata hivyo, mipango yao, ikasitishwa “kiaina” baada ya kuingia kwa John Magfuli. Yeye akarejea kwenye nguvu ya maji kuzalisha umeme.

Ikumbukwe kuwa kwa miaka zaidi ya nane, Tanzania haikuwa na chanzo chochote kipya cha kuzalisha umeme kilichoingia kwenye grid ya taifa.

Suala la kuwepo kwa vyanzo vipya na mifumo imara ya kuzalisha na kusambaza umeme, katika Tanzania, linaamriwa na wanasiasa zaidi, hivyo kulaumu Tanesco ni kuwaonea tu.

HONGERA PROF. MWANDOSYA



Ua likiwa limechomoza katikati ya majani kama lilivyokutwa na kamera ya Prof. Mark Mwandosya wiki iliyopita, huko eneo la Lufilyo, Busokelo, Rungwe, mkoani Mbeya. Pambazuko linampongeza kiongozi huyo mstaafu kwa kuwa na jicho la picha.

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



*Unapona wenzako wanafanikiwa, acha chuki dhidi yao, kikubwa waombe waendeleo kuwa na heri kwani siku moja, huenda neema zao zikakugusa wewe ama baadhi ya ndugu zako; kwa njia moja ama nyingine –
Msemo wa Wahindu.*

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeweza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



Msingi ya haki za binadamu

Na Manace NDOROMA

Haki za Binadamu ni nini?

HAKI za binadamu ni haki ambazo mtu anazipata mara tu anapozaliwa, na anaendelea kuwa nazo hadi kifo chake.

Kwa maneno mengine, kitendo cha kuzaliwa ukiwa mwanadamu na siyo kiumbe kingine, kinakupa moja kwa moja haki fulani ambazo viumbe vingine havina.

Ndiyo maana haki za binadamu zipo tu, hata kama hazijaandikwa popote, tofauti na haki za kisheria ambazo huanza pale sheria husika inapotungwa, na hufika tamati pale ambapo sheria husika imefutwa.

Mifano michache ya haki za binadamu ni pamoja na haki ya kuishi, haki ya kuwa na makazi, haki ya kutoadhibiwa bila kusikilizwa, haki ya mtu kwenda anakotaka, haki ya kutodhalilishwa na kutwezwa kwa utu, haki ya kumiliki mali, nk.

Kutokana na umuhimu wake, katika nchi mbalimbali, haki za binadamu zimewekewa mifumo maalum ya kuzilinda na kuhakikisha hazivunjwi hovyo hovyo.

Katika nchi ya Tanzania kwa mfano, ipo Tume ya Haki za Binadamu na Utwala Bora ambayo iliundwa mwaka 2001 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kila mtu, awe kiongozi ama raia, anaheshimu haki hizo.

Aidha, Haki za Binadamu zimeingizwa rasmi katika Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wameeleza kwa ufasaha kwamba Katiba imeingiza vifungu hivyo kwa mkono wa kulia na kuviondoa kwa mkono wa kushoto.

Maana yake ni kwamba katika Katiba hiyohiyo, zipo ibara zinazomhakikishia kila mtu kulindiwa uhai, heshima na utu



wake, lakini katika vifungu hivyo hivyo, au vingine katika katiba hiyohiyo, vinaweka masharti magumu kwa mtu kuweza kufaidi haki hizo.

Kilichoisukuma jumuia ya kimataifa kuhakikisha kunakuwa na mifumo thabiti ya Ulinzi wa Haki za Binadamu, ni mateso na uhalifu mkubwa dhidi ya binadamu uliofanyika wakati wa vita vya pili vya dunia vilivyoanza Septemba 1, 1939 na kumalizika Septemba 2, 1945.

Ni vita hivi vilivyoshuhudia unyama wa hali ya juu unaoweza kufanywa na mwanadamu dhidi ya mwanadamu mwingine, hususan yule aliye dhaifu kimamlaka, kinguvu, kiuchumi, kisiasa, nk.

Kwa hiyo, mwaka 1948 mataifa yapatayo 50 chini ya mwavuli wa Umoja wa Mataifa yalikutana na kutengeneza orodha ya mambo ambayo yalikuja kufahamaika, kama Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu.

Kwa ujumla, haki za binadamu ni kitu ambacho kila mtu anapaswa kuwa na ufahamu wa asili wa kujua kama zimevunjwa ama hazijavunjwa.

Haki za binadamu zinahusu usawa, heshima, staha, utu na utashi.

Mwandishi wa makala haya ya elimu ni wakili wa kujitegemea anayepatikana Dar es Salaam, Tanzania.

Mapitio ya Kitabu

Uhuru wa habari na yanayotajwa na Kitabu cha ‘Mhariri Msalabani’

Na Esther MNGODO

MARA nyingi waandishi wa habari hudhani kwamba changamoto wanazopitia, kama kukosekana kwa uhuru, ni mpya. Kitabu hiki kinatonesha kwamba changamoto hizi si mpya na zimekuwepo siku zote.

Nimelifahamu jina la Ben Mtobwa tangu nikiwa shuleni. Riwaya yake ya ‘Zawadi ya Ushindi’ ilimpa umaarufu mkubwa miongoni mwa wanafunzi kwani ilisomwa katika mfumo wa NECTA.

Zaidi ya kitabu hicho, nilikuwa sijasoma vitabu vyake vingine mpaka hivi karibuni nilipokikuta kitabu hiki, Mhariri Msalabani: Siku Mia Moja na Hamsini za Mateso katika Maisha Yangu kwenye duka la vitabu la Kase, mjini Arusha; nilifurahi sana.

Enzi za uhai wake, Ben Mtobwa alikuwa mwandishi wa habari. Ndani ya kitabu hiki kilichochapishwa mwaka 2000, Mtobwa anaelezea jinsi ambavyo siku moja aliingia matatizoni kwa sababu ya kazi yake kama mwandishi wa habari. Mtobwa aliheshimika kama Mhariri Mtendaji na mmiliki wa gazeti la Heko, pamoja na kampuni ya uchapishaji ya Heko Publishers.

Katika kitabu hiki kidogo, chenye takriban kurasa 62 tu, Mtobwa anatupeleka kwenye miaka ya tisini na kutuonesha, japo kwa kifupi sana, hali ya uandishi wa habari ilivyokuwa katika muktadha wa kusimamia haki za binadamu na utawala bora.

Shutuma za wizi

Tunapokutana na Mtobwa ni Julai 30, 1999, akiwa ana umri wa miaka 41. Katika mwaka huo, Mtobwa anakamatwa kwa kosa ambalo ukilisikia haiingii akilini: anashutumiwa kwa wizi wa vifaa



vya ofisini. Mahakama ndiyo inayoweza kuamua kama aliiba au la, na kwa hakika, alipelekwa huko mahakamani.

Kama ilivyo ada, wanaanzia kwanza kituo cha polisi. Humo ndani anatupwa ‘shimoni,’ sehemu ambayo, kwa maelezo mafupi anayoyatoa mwandishi, yanakupa picha kuwa si sehemu ambayo ungependa kuingia hata kwa nusu sekunde.

“Baada ya nusu saa,” Mtobwa anaandika kwenye ukurasa wa tano wa kitabu chake, “ilipatikana idadi ya kutosha ya wahalifu. Tukaongozwa na polisi mmoja kupelekwa shimoni, suruali zikiwa zimelegea kwa njaa na kukosa mikanda, miguu ikiwa wazi, huku tukichungwa kama mifugo. Nilijiona kama niliyeanza safari ya ahera, iliyojaa mateso na aibu.”

Mapitio ya Kitabu

Uhuru wa habari na yanayotajwa na Kitabu cha ‘Mhariri Msalabani’

Inatoka Uk. 6

Kama hayo hayatoshi, anasema: “Umenyang’anywa viatu vyako bila maelezo yoyote, huku ukilazimika kutembea juu ya ujiuji wa kitu ambacho hujui kama ni maji, mkojo au matapishi na kulazimika kwenda hivyo chooni ambako ni bahari ya mkojo unaonuka vibaya tokea mlangoni, unaanza kupata hofu kama utatoka humo ukiwa hai.”

Kama ilivyo kwa mwandishi yeyote mdadisi, Mtobwa alitumia tukio hili kama fursa ya kudadisi mfumo wa haki na sheria unavyofanya kazi. Inahamama kutoka kutumia nafsi ya kwanza katika simulizi yake kwenda nafsi ya pili, ambayo huwa haitumiki sana, kana kwamba anajaribu kuweka umbali kati yake na kile kilichomtokea.

Siyo mara ya kwanza

Haikuwa mara yake ya kwanza kuingia shimoni, anakiri hivyo yeye mwenyewe. Mara ya kwanza ilikuwa kwa sababu ya habari iliyoandikwa na Godfrey Mhando kwenye jarida la Mwanamama kuhusu biashara ya picha za wanawake wasio na nguo iliyoshamiri jijini Dar es Salaam wakati huo.

‘Wakubwa’ hawakuifurahia habari hiyo. Kwa kuwa Heko ilichapisha jarida hilo, Mtobwa naye akaswekwa ndani. Heko iliwahi pia kufungiwa na Serikali kwa madai kuwa ilifanya ‘uchochezi’ kwa kuchapisha maoni ambayo ‘yanguweza kuhatarisha amani.’

Lakini kuhusu mashitaka haya yaliyompa mateso mpaka akayaandikia kitabu, Mtobwa hakuelewa kwa nini yalikuza kwa jinsi yalivyokuzwa. Kama ni stakabadhi ya malipo, alikuwa nazo; ushahidi mwingine uliohitajika, aliutoa. Hata hivyo, bado alionekana mwenye makosa.

Kilichomshtua zaidi ni pale ambapo

hakimu mmoja alimuuliza, “Vipi, kwani kesi hii ni ya uhaini?” Swali hili lilitokana na masharti magumu ya dhamana aliyokuwa amepewa Mtobwa.

Bila shaka kumekuwa na maendeleo makubwa katika tasnia ya habari nchini Tanzania kati ya wakati Mtobwa alipokuwa akifanya kazi na sasa. Zimetungwa sheria mbalimbali, ikiwemo Sheria ya Huduma za Habari ya 2016; pia, kumekuwa na maboresho mbalimbali ya sheria hiyo, na zingine zinazotumika na wanahabari.

Hata hivyo, tafakuri ya Mtobwa kutokana na alichokipitia inaendelea kuwa na hoja leo hii, zaidi ya miaka 20 baadaye.

Nafasi ya uandishi

Mtobwa anadadua nafasi ya uandishi wa habari kwa kueleza mchango wake na wa gazeti lake nchini Tanzania, akiandika: “[Kwa] kujenga daraja la kisiasa mara tu mfumo wa vyama vingi ulipoingia nchini na kuwapa uwanja mpana wanaoitwa wapinzani huku chama tawala wakiendela kupata haki yao.”

Mtobwa anaonesha jinsi mwandishi wa habari anaweza kuisababisha serikali kubadilisha msimamo wake juu ya mambo yanayoathiri nchi. Anasikitishwa na waandishi waliokuwa wakiandika kuhusu

Inaendelea Uk. 16

Kumradhi

Katika toleo la Pambazuko Knamba 0062, kwenye ukurasa huu wa saba, kulichapishwa picha ambayo ilikuwa na maelezo yasiyokuwa yake. Tunaomba sana radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza - Mhariri

Habari

Maeneo ya shoroba kupimwa, kulindwa

Mwandishi WETU

SERIKALI ya Tanzania inakamilisha mchakato wa kuanza kupima na kunda maeneo yote ya shoroba ili kuepusha migogoro na wananchi.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kiuruki amesema kuwa maeneo 20 ya mapito ya wanyamapori (shoroba) kati ya maeneo 61 ambayo yalikuwa yametengwa, yatapimwa na kuanza kulindwa.

Mkakati huo pia unalenga kupunguza migogoro baina ya wanyamapori na binadamu nchini.

Miongoni mwa maeneo hayo ni shoroba ya Kwakuchinja iliyopo katikati mwa hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara.

Akizungumza katika Tamasha la Utalii wilayani Same, Kilimanjaro, Kairuki alisema uvamizi maeneo ya shoroba licha ya kuathiri wanyamapori, lakini pia unasababisha migogoro baina ya binadamu na wanyamapori.

Alisema wizara yake inakusudia kubainisha maeneo yote ya shoroba kwa kupimwa na kulindwa.

Alisema wizara katika kupunguza migogoro ya wanyamapori wanaotoka hifadhini, inaendelea na utafiti kubaini sababu za wanyamapori kutoka hifadhini na kwenda kuvamia maeneo ya mashamba na hata makazi ya watu, na kusababisha vifo vya binadamu.

Hata hivyo, alisema maeneo mengi ambayo yana migogoro baina ya wanyamapori na binadamu, ni yale ambayo kuna mapito ya wanyamapori na yamevamiwa kwa shughuli za binadamu ikiwepo kilimo na makazi.

Pamoja na ahadi hiyo, pia serikali imeeleza kuendelea kuelimisha wananchi juu ya kuzuia uvamizi maeneo ya shoroba.

Katika hatua nyingine, serikali imeahidi kutangaza viwango vipya vya vifuta jasho kwa wananchi walioathirika na maafa ya wanyamapori nchini.

Waziri Kairuki alisema tayari wizara



Waziri Kairuki akiwa kwenye gari (mbele) kutembelea maeneo ya shoroba huko Tarangire. Aliyeketi kulia ni Kamishna wa Uhifadhi Tanapa, Juma Ikuji. (Picha na Mpigapicha Wetu).

yake, imewasilisha Wizara ya Fedha kiwango walichopendekeza cha fidia na kwamba wananchi watajulishwa karibuni.

“Kama serikali hatufurahii kuona tembo hao wanakuja kumjeruhi mtu yeyote au kupoteza maisha ya wananchi wetu, tunachokifanya hivi sasa chini ya maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan tunaangalia kiini au chanzo kinachofanya tembo watokea hifadhini na kuingia kwenye makazi ya watu ni nini,” alisema

Alisema serikali hata hivyo imeendelea kulipa fidia kwa wanapata adha za wanyamapori ambapo kwa miaka mitano imetoa zaidi ya Sh. bilioni 5.9 kama kifuta jasho na kifuta machozi.

“Serikali haiwezi hata kidogo kufidia uhai wa mtu kwani hakuna thamani kwa mwanadamu hivyo tunachokifanya sasa ni kulipa kifuta jasho “alisema

Alisema kwa wale ambao mazao yao yameathirika kutokana ana mwingiliano wa wanyamapori, tayari serikali imetoa Sh bilioni 1.2.

Waziri Kairuki alisema, zaidi ya Sh milioni 462 kwa sasa zipo katika uhakiki na kadri fedha hizo zitakapopatikana zitalipwa mapema iwezekanavyo kwa wananchi wanaohusika.

Awali Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Alhaji Juma Ikuji alisema shirika lake litaendelea kuboresha mazingira ya hifadhi ili kuvutia watalii na kupunguza migogoro baina ya wanyamapori na binadamu.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Makundi yatakayomsumbua Dkt. Nchimbi

Na Rashid MTAGALUKA

TANGU Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi tateuliwe na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuvaa 'viatu' vya Daniel Chongolo katika nafasi ya ukatibu mkuu, mengi yamezungumzwa na wachambuzi wa siasa.

Hata hivyo, nami napenda kuzungumzia namna Dkt. Nchimbi atakavyomudu kuishi na kuyapatanisha makundi makubwa matatu ndani ya chama chake.

Kuna kundi mimi naliita CCM-Asilia. Hili ni kundi la kwanza lililosheheni wanachama wengi wakongwe waliyoishuhudia CCM ikizaliwa kutoka kwa TANU na ASP.

Wafuwasi wengi wa kundi hili, wakiwa ni wazee kwa sasa - hawafurahii mabadiliko ya mara kwa mara ndani ya chama hicho. Wanataka mambo yanayojadiliwa kwenye vikao yaishie ndani ya vikao, wanashangaa hata majina ya wanaokuja kuteuliwa kwa nafasi mbalimbali na chama ama serikali, yanavuja mtaani kabla hayajatangazwa!

Kundi hili siku zote limekuwa haliridhishwi na mwenendo mpya wa siasa kwa wana CCM kuwa 'chawa' wa viongozi badala ya chama, na linastaajabu kuona baadhi ya vijana waliowavunjia heshima hadharani, baadhi ya wazee walioitumikia serikali katika ngazi ya kitaifa, wakiambiwa kupewa nafasi za juu za uongozi.

Tatizo kubwa la kundi hili ni kukosa mtu shupavu mwenye ujasiri wa kuzungumza kwa uwazi hayo wanayochukizwa nayo kwa sasa. 'Wanaumia ndani kwa ndani.'

Aidha, lipo kundi jingine kubwa lenye nguvu, mimi naliita CCM-Mageuzi. Kundi hili linatambulika zaidi kwa tabia ya wafuasi wake kuwa na misimamo thabiti isiyoyumba.

Tabia ya kundi hili ni pamoja na kutaka mabadiliko yoyote yatakayoonekana yana



Dkt. Nchimbi

tija, yawekewe kanuni kwenye chama.

Kwa mfano, kuna hili la kiongozi aliyeko madarakani hasa ngazi ya rais inapofika awamu ya pili asipingwe, lakini halipo kwenye katiba wala kanuni, kwa hiyo wana mageuzi wanasema huyu mtu apingwe ndiyo kipimo chake cha miaka mitano amefanya nini.

Wanaongeza kusema kuwa, kama wanataka asipingwe, basi iwekwe kwenye kanuni, na ikionekana mtu amevuta fomu ya kugombea nafasi hiyo kwa maana ya kumpinga, asionekane ametenda dhambi!

Halafu kuna kundi la CCM-Kindakindaki, hawa ni wafia chama; inyeshe mvua, liwake jua, lakini wao wapo CCM. Hawa wakati mwingine wako tayari hata kufunga 'goli la mkono' ikionekana kufanya hivyo kutakivusha chama chao!

Swali langu, Nchimbi atahimili mikikimikiki ya makundi haya matatu na hususan wana-Kindakindaki ambao inadaiwa wamesajili mpiga zumari mahiri anayeimba nyimbo tamu zinazomfurahisha mlipa ujira?

Rashid Mtagaluka ni Mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu namb: 0784 438 546; au Barua-pepe: /mtagaluka@gmail.com

Kenya

Mapazia ya 183m/ yaning'inia ofisi ya Gachagua

Na Mwandishi WETU,
Nairobi

WAKATI uongozi wa juu wa Kenya, ukiongozwa na Rais William Ruto ukijitanabaisha kuwapigania wanyonge, matumizi makubwa ya serikali hiyo, yanapingana na falsafa hiyo.

Kwamba badala ya fedha nyingi kuelekezwa kutatua changamoto za Wakenya wengi masikini, “wakubwa” wanafanya matumizi makubwa katika ofisi zao, kwa gharama za walipa kodi wa nchi hiyo.

Pamoja na viongozi wa juu; rais, naibu wake, mawaziri na wakubwa wengine serikalini, sasa imebainika kuwa kuna harufu ya ufisadi katika kuhudumia ofisi zao.

Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Kenya, Nancy Gathungu, iliyoonwa na Pambazuko jana, imefichua kuwa Ofisi ya Naibu Rais Rigathi Gachagua, imepambwa kwa mapazia yaliyonunuliwa kwa Shilingi za Tanzania milioni 183 (sawa na Shilingi ya Kenya milioni 10.27). Fedha hizi ni sawa na dola za Marekani 72,000. Mapazia hayo yalinunuliwa mwaka jana, 2023.

Watu kadhaa waliozungumza na Pambazuko katika mitaa ya Nairobi jana, wamesema ofisi hiyo ya Gachagua, ingeweza kuwa na mapazia ambayo hayahitaji kiasi kikubwa namna hiyo cha fedha ambazo zingeweza kufanya kazi nyingine za maendeleo yanayogusa maisha ya Wakenya wengi.

Pambazuko limebaini kwamba kiasi hicho cha Shilingi za Kenya milioni 10.27 zingeweza kutumika kununua nyumba 12 ambazo ziko katika mpango wa nyumba nafuu kwa watu wenye uwezo mdogo wa kiuchumi.

Nyumba moja katika mpango huo maarufu kuwa ni mradi wa kijamii, huuzwa kwa Shilingi za Kenya 840,000.



Gachagua

Mpango huu unalenga zaidi Wakenya wenye mapato ya chini ya KSh. 20,000 kila mwezi.

Pia imebainika kuwa gharama za mapazia hayo zingeweza kutosha kununua nyumba 10 katika mpango wa nyumba nafuu kwa watu wenye kipato kisichozidi Ksh. 150,000 kwa mwezi.

Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali inafuatia matokeo ya ukaguzi ya Msimamizi wa Bajeti ya Kenya (CoB), Margaret Nyakang'o ambaye aling'amua kuwepo kwa matumizi makubwa ya Serikali Kuu kwa makazi ya viongozi wakuu, ambapo ilibainika kutumika kwa Shilingi za Kenya (Ksh) milioni 600 mwaka jana kugharimia ukarabati wa makazi rasmi ya Gachagua, Mtaa wa Karen, Nairobi.

Wananchi wengi waliohojiwa na Pambazuko wanaeleza kuwa matumizi haya makubwa yanaibuliwa sasa katikati ya wimbi kubwa la kuongezeka kwa gharama za maisha, huku idadi kubwa ya Wakenya, wakishindwa kuzimudu na kuishia kula mlo mmoja au kukosa kabisa.

Kwa upande wake, Rais Ruto na wasaidizi wake wanaendelea kudai kuwa uchumi wa nchi hiyo unaimarika zaidi kwa kuwa bei za vyakula zimepungua na kuimarika kwa thamani ya shilingi ya Kenya dhidi ya dola ya Marekani.

Sera ya Jinsi yaibua 'sura kakamavu' ACT

Na Mwandishi WETU,
Zanzibar

SERA ya Jinsi inayolenga kuhamasisha ushiriki mpana wa viongozi wanawake kwenye vyombo vya uamuzi ndani ya Chama cha ACT-Wazalendo, imechochea ushindani mkali dhidi ya wanaume.

Idadi kubwa ya wanawake wamejitokeza kutaka kushika nafasi mbalimbali za juu kwenye uongozi wakishindana na wanaume maarufu.

ACT-Wazalendo, chama kilichoanzishwa mwaka 2014, kinatarajiwa kufanya mkutano wake mkuu wa taifa wiki ya kwanza mwezi ujao, Machi, ambako Dorothy Semu ameamua kujitosa kuwania kukalia kiti kinachoachwa na Zitto Zuberi Kabwe anayestaafu wadhifa wa Kiongozi wa Chama (KC) aliushika tangu mwaka 2014.

Akiwa ndiye mwanamke nguzo kubwa ya chama katika kusimamia sera yake mpya ya kuzingatiaji wa masuala ya jinsi, iliyopitishwa hivi karibuni na Kamati Kuu, Semu anaachia nafasi ya makamu mwenyekiti wa chama hicho, na kujiandaa kukabiliana na Mbaralah Maharagande. Wote tayari wamerudisha fomu za kuwania nafasi hiyo.

Maharagande ambaye aligombea ubunge Morogoro Mjini uchaguzi wa 2020, amekuwa mjumbe wa Kamati Kuu na msemaji kivuli wa masuala ya haki za binadamu kwenye serikali kivuli ya chama hicho.

Wanawake wengine mbalimbali wamejitokeza kuomba nafasi za kuwa wajumbe kwenye Kamati Kuu na Halmashauri Kuu Taifa wakiwakilisha kanda za maeneo wanakotoka, ukiacha wale wanaotaka kuongoza wanawake wenzao katika Ngome ya Wanawake.

Mwanamama mwingine, Halima Nabalang'anya, ambaye ni waziri kivuli



Dorothy Semu

wa viwanda na biashara, anagombea ujumbe wa Kamati Kuu.

Severine Mwijage, Mbunge wa zamani wa jimbo mkoani Kagera kupitia Chama cha Wananchi (CUF), ameingia kuwania uenyekiti wa Ngome ya Wanawake, akisimama na mwenza wake Miza Bakari Haji, mwanamke mwingine kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Ili kuitwaa nafasi hiyo kwenye ngome, wawili hao watakuwa na kibarua kizito kushindana na Janeth Rithe, naibu katibu wa habari na uenezi wa chama hicho taifa.

Wapo wanawake kadhaa walioingia kutaka nafasi za ujumbe kwenye Ngome ya Wazee pamoja na ile ya Vijana, wakiongozwa na Rukkaya Mohamed Rashid anayewania uenyekiti wa vijana, nafasi ambayo Abdul Nondo amesimama kidete kuitetea.

Nondo anayekalia kiti hicho tangu mwaka 2019, anakabiliwa na upinzani mkubwa kutoka kwa vijana wenzake akiwemo Ntakije Ntanena anayesimama na Abdul Malik Juma. Julius Massabo pia anagombea.

ACT- Wazalendo inayojipatia maarufu kwa kuvutia wanawake wanaopewa nafasi katika uongozi, ilipitisha sera mahsusi ya jinsi ikilenga kutoa uwakilishi sawa na wanaume 50/50 kwenye uongozi ikiwa ni chama cha kwanza kutekeleza itifaki za kikanda.

Habari

Mgawo umeme kuwa historia?

Na Tryruckia MFINANGA

HUENDA historia mbaya ya nchi kuwa gizani – kwa kukosa umeme wa uhakika, sasa ikakoma, baada ya kuingizwa kwa nishati zaidi kwenye gridi ya taifa.

Jana, jumla ya megawati 235 ziliingizwa kwenye mfumo wa kusambaza umeme kwa Watanzania waliokuwa wakilalamika kuwepo mgawo wa umeme kwa muda mrefu sasa.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko amesema jana kuwa, mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) wenye uwezo wa megawati 2,115 umeanza kazi na kuingiza megawati 235 katika gridi ya Taifa kupitia mtambo namba 9.

“Hatua hii ni utekelezaji wa ahadi ya serikali kuwa mtambo huo ungeanza kuzalisha umeme tarehe 25 Februari, 2024, ahadi iliyotimizwa siku tatu kabla kuanzia tarehe 22 Februari 2024 mtambo huo ulipoanza uzalishaji,” amesema.

Dkt. Biteko amesema hayo wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwa baadhi ya wakuu wa vyombo vya habari na wahariri katika eneo la mradi wilayani Rufiji, Pwani.

Wahariri waliotembelea eneo la mradi, walipata fursa ya kufika maeneo mbalimbali ikiwemo bwawa la kuhifadhi maji yatakayozalisha umeme, tuta kuu na mitambo mingine ya umeme.

Dkt. Biteko ameeleza kuwa, kuingia kwa megawati 235 kwenye gridi ya taifa kumeboresha hali ya kupatikana umeme nchini na kupunguza upungufu wa umeme kwa zaidi ya asilimia 85.

Ameongeza kuwa utekelezaji wa Mradi Bwawa la Julius Nyerere unaendelea na ifikapo Machi 2024, megawati nyingine 235, zitaingia katika gridi kupitia mtambo namba 8 na kufanya JNHPP kuingiza megawati 470 kwenye gridi na hivyo kufanya nchi kuwa na ziada ya umeme ya megawati 70.

“Utekelezaji wa mradi huo ni jitihada za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye alikuta mradi huo ukiwa na asilimia 33 na sasa mradi huo unafikia mwisho,” ameongeza.

Pamoja na kuingizwa kwa megawati hizo, Dkt. Biteko amesema Rais Samia amehimiza TanESCO kuendelea kuibua na kuendeleza



Dkt. Biteko akitangaza kuingizwa kwa megawati 235 kwenye gridi ya taifa jana. Picha kutoka Tanesco.

Mgawo umeme kuwa historia?

Inatoka Uk. 12

vyanzo vipya vya umeme ikiwemo gesi, maji na nishati jadidifu inayojuumuisha jua, upepo na jotoardhi.

Dkt. Biteko pia amepongeza juhudi za serikali ya awamu ya tano iliyoongozwa na Dkt. John Magufuli kwa uamuzi wa kutekeleza mradi huo ambao ulianza kutekezwa mwaka 2018.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko ameeleza kuwa, utekelezaji wa JNHPP hauifanyi wizara ya nishati na taasisi zake kubweteka na kutegemea umeme kutoka mradi huo pekee, bali kasi ya utekelezaji wa miradi mingine mipya inaendelea.

Miradi mingine ya kuzalisha umeme ni pamoja na Rumakali (222MW), Ruhudji (358) na miradi ya jotoardhi ya Ngozi na Kiejo-Mbaka pamoja na mradi wa umeme jua wa Kishapu (150MW).

Naibu waziri mkuu huyo amehimiza Tanesco kuhakikisha kuwa wananchi wanaozunguka maeneo yenye mitambo ya kuzalisha umeme, wanapata nishati hiyo na bila changamoto kwa kuwa hao ndio walenzi wa maeneo hayo na mradi wenyewe.

Dkt. Biteko amepongeza Shirika la Ugavi wa Umeme (Tanesco) na kampuni ya usimamizi wa mradi ya TECU kwa kutekeleza na kusimamia vyema mradi ambao umewezesha kuingiza megawati 235 kwenye gridi.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso ambaye aliambatana na Dkt. Biteko amesema kuwa ujazo wa maji unaohitajika katika Bwawa la JNHPP ni mita za ujazo bilioni 32.7 na sasa kuna mita za ujazo bilioni 28, hivyo bado mita nne tu bwawa hilo kujaa kabisa.

Amesema kuwa makadirio ni kuwa mita nne zilizobaki zitajaa karibuni kupitia usimamizi madhubuti wa Bonde la Maji la Rufiji.

Aweso ametoa mwito kwa wananchi kutunza vyanzo vya maji na kutofanya uharibifu wa mazingira ili kupatikana

kwa nishati kuwa ni endelevu na kudumu.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge amesema kuwa mradi huo ni muhimu katika kutekeleza dhamira ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuifanya Pwani kuwa mkoa wa kimkakati kwa kujenga viwanda vingi zaidi ambavyo kufanya kwake kazi kunategemea nishati ya umeme wa uhakika.

Amesema kuwa, mahitaji ya umeme mkoani Pwani ni megawati 130, lakini bado hayatoshelezi mahitaji, hivyo mradi wa JNHPP kupitia kituo cha umeme cha Chalinze kitawezesha mkoa huo kupata umeme wa uhakika ambao utachochea wawekezaji wapya.

Ameongeza kuwa, kwa sasa Mkoa wa Pwani una viwanda 1,533 ambapo katika serikali ya awamu ya sita, viwanda 30 vinajengwa huku 17 vikiwa ukigoni kumalizika, hivyo umeme wa uhakika ni muhimu katika kufanya viwanda hivyo kufanya uzalishaji.

Meneja Mradi wa JNHPP kutoka kampuni zinazotekeleza mradi huo (Arab Contractors na Elsewedy Electric) Mohamed Zaky, amesema kuwa kampuni hiyo inaona fahari kufikia hatua hiyo ya uzalishaji na kwamba nia yao ni kutimiza ndoto ya Tanzania kuzalisha megawati 2115 kupitia mradi wa JNHPP.

Aidha, amepongeza Dkt. Biteko kwa msukumo anaoutoa kwa wakandarasi hao ili kutekeleza mradi kwa wakati na pia kwa kuusimamia kwa karibu mradi husika.

Viongozi wengine walioambatana na Dkt. Biteko ni Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu Mteule Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga, Mwenyekiti wa Bodi ya Tanesco, Dkt. Rhimo Nyansaho na mkurugenzi mtendaji wa shirika hilo, Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga.

Tangazo



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au

Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Rais Museveni akutana na timu yake



Rais wa Jamhuri ya Uganda, Yoweri Museveni, ambaye pia ni mwenyekiti wa chama chake cha NRM, amekutana na uongozi wa sekretarieti ya chama hicho Ikulu, Entebbe. Wajumbe walimweleza kiongozi huyo kuhusu maandalizi ya uchaguzi ujao wa ndani ya chama utakaofanyika hivi karibuni. (Picha zote na Ikulu).



Rwanda

Mtuhumiwa mauaji ya kimbari adakwa

Na Mwandishi TRT

BAADA ya kukimbia mkono wa sheria kwa zaidi ya miaka 30, hatimaye mmoja wa washukiwa wa mwisho katika mauaji ya kimbari ya Rwanda, amekamatwa.

Mtuhumiwa huyo ambaye amedakwa akiwa nchini Afrika Kusini, anatakiwa kurejeshwa Rwanda ili kuendelea na kesi inayomkabili.

Hata hivyo, mtuhumiwa huyo, Fulgence Kayishema, ameomba aendelee kusalia nchini humo kwa kuwa anahofia maisha yake akiwa Rwanda.

Kayishema anakabiliwa na mashitaka ya kupanga na kutekeleza vifo vya watu waliokuwa wamehifadiwa ndani ya Kanisa Katoliki ili kuepuka kuuawa.

Inaelezwa kuwa yeye pamoja na watu wengine, walipanga mauaji ya kikatili ya baadhi ya mamia ya maelfu ya watu katika mauaji ya kimbari ya Rwanda takriban miaka 30 iliyopita.

Alikamatwa Jumanne iliyopita na wakili wake anadai kuwa endapo kutakuwepo na uamuzi wa kurejeshwa Rwanda, hakutakuwa na kizuizi.

Kayishema, ofisa wa zamani wa Jeshi la Polisi Rwanda, ni mmoja wa watoro wanne wa mwisho wanaotafutwa na Mahakama ya Kimataifa ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya mauaji ya kujibu tuhuma za mauaji ya kimbari na uhalifu dhidi ya ubinadamu.

Inaelezwa kuwa katika mauaji hayo ya kimbari zaidi ya watu milioni moja walipoteza maisha ndani ya siku 100 za mapigano. Mauaji hayo yalitokea mwaka 1994.

Mtuhumiwa huyo amekanusha kuhusika na ghasia wakati wa mauaji ya halaiki, lakini ameomba samahani kwa mauaji hayo.



Fulgence Kayishema

Uhuru wa habari

Inatoka Uk. 7

yaliyomkuta kwa kuangazia upande mmoja; na kusema kuwa “mwandishi anaelezewa kama kioo cha taifa, siyo tarumbeta au kasuku wa taifa.”

Ni rahisi kudhani kwamba changamoto tunazoziona katika tasnia zilianza na sisi. Tunadhani kwamba changamoto za uhuru wa vyombo vya habari zimeibuka tu sasa, na pengine huko nyuma kulikuwa na ahaueni; lakini ni muhimu kujifunza kutokana na historia kwani kila kitu kilichowahi kuwa, kitakuwa.

Mtobwa hakuishia ‘shimoni’ tu, alifika hadi gerezani huko Mwanza. Akiwa huko anakutana na mengi ambayo huwa hayafahamiki kwa urahisi nje ya gereza. Mtobwa anaangazia haki za wafungwa kwa kina – jinsi ambavyo hali zao za kiafya huzorota kwa lishe duni, hali ya uchafu, kupigwa, na manyanyaso mengine.

Esther Karin Mngodo ni mwandishi anayeishi Dar es Salaam, Tanzania. Unaweza kumpata kupitia mtandao wa X kama @Es_Taa. Makala haya yamechukuliwa The Chanzo ambako yamechapwa kwa mara ya kwanza. Pambazuko inayatumia kwa sababu maalum.

Ujerumani kulipa fidia mauaji ya kimbari

Na Mwandishi MAALUM

WANANCHI wa Namibia wameendelea kuishinikiza serikali yao kuibana Ujerumani kulipa fidia kwa mauaji iliyofanya wakati 'ikiikalia' nchi yao.

Wanaeleza kuwa Ujerumani wakati ikiitawala Namibia iliendesha ubabe mkubwa uliosababisha idadi kubwa ya wananchi kupoteza maisha. Mauaji hayo yanaelezwa kuwa ni ya kimbari.

Tayari Ujerumani imekiri kwamba mauaji yaliyofanywa na wanajeshi wake wakati wa ukoloni nchini Namibia yalifanana na mauaji ya halaiki, lakini bado haijaomba msamaha rasmi wala kulipa fidia.

Wananchi wa Namibia wamemtaka Rais wa Ujerumani Frank-Walter Steinmeier kuharakisha mazungumzo juu ya fidia kwa mauaji ya kimbari ya wakati wa ukoloni yaliyofanywa na wanajeshi wan chi yake.

Rais wa Ujerumani alikuwa Windhoek, mji mkuu wa Namibia, kutoa heshima kwa Rais wa Namibia, Hage Geingob, aliyefariki Februari 4 na kuzikwa jana – Jumapili.

Alikumbushwa hayo wakati wa ibada ya kumbukumbu siku ya Jumamosi kwamba Ujerumani bado haijakubaliana juu ya fidia kwa mauaji ya watu wa makabila makubwa ya Herero na Nama kuanzia 1904 hadi 1908.

Mei 2021, Ujerumani ilikubali kwamba mauaji yaliyofanywa na wanajeshi wake yalikuwa sawa na mauaji ya halaiki na imejitolea kufadhili miradi ya maendeleo kwa gharama ya euro bilioni 1.1 (dola bilioni 1.2) kwa miaka 30. Hata hivyo, hadi sasa, taarifa zinaeleza kuwa hakuna fedha zilizolipwa.

Kwa wananchi wengi wa Namibia, ikiwa ni pamoja na baadhi ya maofisa wakuu, ofa hiyo haitoshi na hailingani na fidia rasmi.

Kabla ya kukumbwa na umauti, Rais Geingob alikuwa akihimzia Ujerumani



Rais Frank-Walter Steinmeier

kuanza kulipa fidia kwa Wanambia kufuatia kadhia hiyo ya mauaji.

Akijibu shutuma msimamo wa Namibia, Rais wa Ujerumani Steinmeier alisema nchi yake imejitolea kuboresha uhusiano na Namibia na kwamba kamwe haiwezi kuacha historian a uhusiano baina ya nchi mbili kutetereka.

“Njia ya upatanisho ambayo tumeianza takriban miaka kumi iliyopita haikuwa rahisi, lakini kwa pamoja tumefika mbali sana na tunataka kufika mbali zaidi,” alisema.

Steinmeier alisema Rais Geingob alimwambia mwishoni mwa mwaka jana – 2023 kwamba alitaka kuweza kutia saini tamko la pamoja la Ujerumani na Namibia ili kuweka makubaliano rasmi kuhusu namna nzuri ya kumaliza “chuki” za wananchi kuhusu mauaji ya kimbari.

“Na unajua, maridhiano siyo kufunga yaliyopita, ni kuchukua jukumu kwa maisha yetu ya zamani na ni dhamera ya maisha bora ya baadaye,” Steinmeier alisema.

“Natumai nitaweza kurejea nchini hivi karibuni na chini ya hali tofauti kwa sababu nina hakika kwamba ni wakati mfafaka wa kuomba msamaha kwa watu wa Namibia kufuatia yale yaliyotokea miaka mingi iliyopita, tena ikiwa ni wakati mbaya wa ukoloni.”

DRC

EU, Rwanda zaangukia tuhuma nzito

Na Mwandishi MAALUM

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) inadai kuwa Rwanda na Umoja wa Ulaya (EU), zimekuwa zikiwaunga mkono waasi wa M23, ambao wamekuwa wakiendeleza mashambulizi ya mara kwa mara mashariki mwa nchi hiyo.

Rwanda na EU zimekuwa zikikana tuhuma hizo kwa maenezo kwamba hazina ukweli wowote unaoweza kuthibitishwa pasipokuwa na shaka.

Kiongozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi amesema yuko tayari kwa mazungumzo na mwenzake wa Rwanda, Paul Kagame, ili kutafuta amani.

Rais Tshisekedi pamoja na kueleza utayari wake wa kuanza mazungumzo na mwenzake wa Rwanda, Kagame, lakini amelaani mkataba wa hivi karibuni kati ya Rwanda na EU ambao unahusu biashara ya madini.

Mkataba baina ya Rwanda na EU unahusu biashara ya madini aina ya tantalus ambayo yanapatikana zaidi DRC. Madini hayo hutumika zaidi kutengeneza bidhaa za kielektroniki.

Rais Tshisekedi anasea kuwa EU na dunia inatambua kwamba madini hayo hayako Rwanda na yanapatikana DRC kwa wingi, sasa iweje kuwepo makubaliano ya kuuza bidhaa ambayo haipo kwa mmoja wao? Alihoji.

"Huu ni uchokozi," amesema Rais Tshisekedi katika mahojiano ya ana kwa ana na waandishi wa habari wa Televisheni ya Taifa ya Rwanda (RTNC), Alhamisi iliyopita.

Rais Tshisekedi ameendelea kuituhumu Rwanda kwamba imekuwa ikifanya mbinu za kuiba madini kutoka nchini kwake kwa kutumia waasi. Rwanda, kama kawaida yake, imekuwa ikikana tuhuma hizo.

"Rwanda haipaswi kuuza utajiri ambao siyo wake," anasema.



Rais Tshisekedi

Waasi wa M23

Rais Tshisekedi anaamini kuwa mapato kupitia mauzo hayo haramu, yatawezesha kuimarisha majeshi yao na kuendelea na malengo yao harama nchini Congo.

Aliituhumu Rwanda kwa kukiunga mkono kikundi cha M23, kinachofanya mashambulizi ya mara kwa mara mashariki mwa Congo.

"Rwanda inaendelea kujificha nyuma ya kivuli cha M23, na ndio maana siko tayari kufanya mazungumzo na kikundi hichi cha magaidi," amesema Rais Tshisekedi wakati akijibu swali la iwapo yupo tayari kufanya mazungumzo na kikundi hicho.

"Kipaumbele changu ni amani, nataka amani ya kudumu kwa nchi yangu, kwa hilo niko tayari kuweka pembeni tamaa zangu za kivita..."

... Kama sote tuko tayari bila vita, nami nitaafiki hilo kwa mikono miwili, lakini kama lithitaji vita, nitafanya hivyo kwa mikono miwili pia," ameongeza.

Rais Tshisekedi pia anaelezwa kuwa na mpango wa kukutana na kiongozi mwenzake wa Angola, Joao Lourenco Februari 27, mwaka huu. Lourenco ni mpatanishi katika mgogoro huu.

Mara kadhaa, Rais wa Rwanda Paul Kagame amekana kuhusishwa na kukiunga mkono kikundi cha waasi wa M23.

Habari hii imepatikana kwa msaada kutoka TRT Afrika.

Mwanariadha mwingine afariki akishiriki mbio

Na Mwandishi WETU

KENYA imepoteza kwa kifo cha mwanariadha mwingine, Charles Kipsang Kipkorir (33), wiki mbili tu baada ya kifo cha Kelvin Kiptum, ambaye alikuwa akishikilia rekodi ya marathon ya juu kabisa duniani.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la China, Xinhua, Kipsang alifariki juzi - Jumamosi, Februari 24, 2024 nchini Cameroon.

Alianguka na kupoteza maisha muda mfupi baada ya kumaliza mashindano ya riadha.

Kulingana na vituo vya habari Cameroon, Kipsang alikuwa anashiriki kwa mara ya 29 ya michuano ya Mount Cameroon Race of Hope.

Alikata roho wakati akiendelea kupokea huduma za dharura hospitalini.

Wakati wa mashindano, Kipsang

alikuwa anaongoza kabla ya kukumbwa na matatizo akikaribia utepe.

Mwanariadha huyo alimaliza mbio akiwa nafasi ya 16 kama ilivyothibitishwa na Gavana wa Cameroon Bernard Okalai Bilia.

Madaktari waliokuwa uwanjani - kwenye Uwanja wa Molkyo walimfanyia huduma za dharura za kitabibu Kipsang kabla ya kumhamishia Hospitali ya Buea Regional.

Akizungumzia tukio hili, Gavana Bilia alishindwa kueleza bayana chanzo cha kifo hicho.

“Hatuwezi kusema hasa nini kilifanyika. Tunaweza kuamini pengine ni mshtuko wa moyo.”

Kisha akaongeza; “walimpeleka hospitali ya kanda, lakini alipofikishwa tulielezwa kuwa tayari amefariki”.

Kipkorir amekua mwanariadha wa kwanza kujisajili katika shindano hilo la kimataifa kongwe zaidi Afrika.

Aliwahi kudhihirisha kipaji chake katika mbio kadhaa duniani zikiwemo mashindano ya masafa marefu ya Bali, the Kuala Lumpur na Casablanca.

Kiptum alifariki jijini Nairobi, katika ajali akiwa na kocha wake Gervais Hakizimana.

Alizikwa eneo la Kaunti ya Elgeyo Marakwet Ijumaa, Februari 23, 2024 katika mazishi yaliyowaleta pamoja viongozi wa hadhi ya juu serikalini na duniani, akiwemo Rais William Ruto, naibu wake, Rigathi Gachagua na Mkuu wa Mwaziri, Musalia Mudavadi.



Yanga hiyooo robo fainali...



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Yanga kutoka Tanzania wakifurahia ushindi baada ya 'kuichakaza' Timu ya CR Belouisdad na kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Klabu Bingwa Afrika. Yanga ilifunga timu hiyo kutoka Algeria kwa maba0 4-0. (Picha kutoka mtandao wa X wa Yanga). Mchezo huo ulichezwa jijini Dar es Salaam, Just - Jumamosi.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

